TANGAZO LA SERIKALI NA. 65 la tarehe 2/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA NSONGWI MANTAJI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Nsongwi Mantaji ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 617 yenye majira-nukta 560925MS, 9013328KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D1 yenye majira-nukta 561004MS, 9012673KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.8 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D2 yenye majira-nukta 560168MS, 9012648KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D3 yenye majira-nukta 560182MS, 9013046KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimajinamba VMA 615 yenye majira-nukta 559720MS, 9012867KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VMA 616 yenye majira-nukta 559657MS, 9013379KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 1.2 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*